

HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz
Tovuti:www.nsimbodc.go.tz



S.L.P 688

MPANDA

Press No: NDC/ICPRU/Press no.15

June 18, 2018

TAARIFA KWA UMMA/VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Wilaya ya Mpanda **Bi.Lilian Charles Matinga** leo Juni 18, 2018 amepokea msaada wa mabati ikiwa ni mchango wa Benki ya NMB kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Bi Matinga amepokea msaada huo wa mabati 360 yenye thamani ya shilingi Milioni 10 kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya nyanda za juu Kusini **Bw.Straton Chilongota** katika tukio la kukabidhi msaada huo lililofanyika katika shule ya sekondari Nsimbo.

Akikabidhiwa msaada huo, **Bi.Lilian Matinga** ameishukuru NMB kwa kuwa mstari wa mbele katika uchangiaji wa shughuli mbalimbali za uboreshaji wa miundombinu ya elimu na kuwataka wadau mbalimbali wa maendeleo Nchini kuunga mkono jitihada za NMB katika uboreshaji huduma za jamii.

Shule zilizonufaika na msaada wa mabati kutoka Benki ya NMB ni shule ya Sekondari Nsimbo na Kenswa zote zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Imetolewa na :

John A.Mganga

Afisa Habari Mawasiliano na Uhusiano (W)
Kitengo cha Habari Mawasiliano TEHAMA na Uhusiano,
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.